**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA SITA

**10 MEI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 10 MEI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

## II. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:-**

**130. MHESHIMIWA ESTER ALEXANDER MAHAWE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Serikali kupitia mpango mkakati wa kuwawezesha Wananchi wa vijijini iliahidi kutoa sh. 50,000,000/= kwa kila kijiji na mtaa:-

(a) Je, ni lini fedha hizo zitatolewa;

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi juu ya njia bora ya kutumia fedha hizo.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 131. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Tangu kuanzishwa kwa Wilaya ya Mbogwe mwaka 2012 Watumishi wa iliyokuwa Wilaya ya Bukombe walihamishiwa Wilayani Mbogwe lakini hawajalipwa stahiki zao za posho ya kujikimu pamoja na zile za usumbufu:-

Je, ni lini Watumishi hao watalipwa stahiki zao.

### 132. MHESHIMIWA BONNAH MOSSES KALUWA (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Katika Jimbo la Segerea kuna zahanati kumi (10) lakini hakuna zahanati hata moja iliyopandishwa hadhi kuwa kituo kikubwa cha Afya chenye uwezo wa kulaza wagonjwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi zahanati ya Tabata 'A' kuwa kituo cha Afya kwa sababu ina miundombinu yote inayofaa kwa kituo cha afya.

**133. MHESHIMIWA ALLY SEIF UNGANDO (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji kwenye Jimbo la Kibiti kwenye maeneo ya Delta kama Nyamisati, Mchinga, Mfisini Kiomboi, Msala, Kiongoroni, Naparoni na Mbuchi:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua tatizo hili.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**134. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kumekuwepo na ahadi nyingi wakati wa kampeni kutoka kwa Marais wa Awamu ya Nne na ya Tano kuwa barabara ya kutoka Mkomazi kupitia Bendera, Kihurio, Ndungu, Maore, Kisiwani hadi Same Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu ahadi hizo.

**135. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Gulwe – Berege – Chitemo – Mima – Sazima – Igoji Kaskazini – Iwondo – Fufu inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ni mbaya sana na inapitika kwa shida sana hasa wakati wa mvua/masika:-

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja kubwa ya barabara hiyo kuhudumiwa na Serikali Kuu (TANROADS) badala ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ambayo uwezo wake kifedha ni mdogo.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**136. MHESHIMIWA ALI HASSAN KING (JANG'OMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la makazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi na Mheshimiwa Rais aligusia azma hiyo alipokuwa akilihutubia Bunge la Kumi na Moja kwenye kikao cha ufunguzi:-

Je, Serikali imepanga kujenga Mikoa mingapi majengo hayo ikiwemo Zanzibar.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

### 137. MHESHIMIWA MUHAMMED AMOUR MUHAMMED (BUMBWINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kumekuwa na unyanyasaji mkubwa unaofanywa na JWTZ wa kuwanyang'anya wavuvi samaki wao licha ya kwamba watu hao wanajitafutia kipato kupitia bahari kama watanzania:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa unyanyasaji huo unaofanywa na Jeshi la Wananchi kwa Wananchi wake.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

### 138. MHESHIMIWA GIMBI DOTTO MASABA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wakazi wengi wa Mkoa wa Simiyu huendesha maisha yao kwa kutegemea kilimo na ufugaji, ambapo Mkoa huo umepakana na maeneo makubwa na mazuri kwa kazi hizo jirani na mbuga ya Serengeti:-

(a) Je, Serikali itatenga lini maeneo ya Kilimo na Mifugo kwenye vijiji vinavyopakana na Mbuga ya Serengeti;

(b) Je, Serikali itathamini lini mifugo na mazao ya Wakulima hawa kama vile inavyothamini wanyamapori wa mbugani kwani huonekana ni halali kwa wanyamapori kuua/kuharibu mazao ya Wananchi wakati si halali Wananchi kuingiza mifugo au kuchimba hata mizizi ndani ya mbuga ya wanyama.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:**

**139. MHESHIMIWA HAFIDH ALI TAHIR (DIMANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo:- Katika Bunge la 2005 – 2010 kulitokea hoja ya TFF kujiunga katika shirikisho la mpira la kimataifa – FIFA bila ridhaa ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; hoja hiyo ilipelekea aliyekuwa Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Pinda kuunda Kamati Maalum yenye wajumbe kutoka ZFA na TFF ili kuondoa utata huo:-

(a) Je, ni nini matokeo ya Kamati hiyo iliyoundwa na Waziri Mkuu;

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutopatikana muafaka au uamuzi uliofikiwa kwa pamoja ni kuchelewesha agizo la Waziri Mkuu;

(c) Je, Serikali inasemaje kuhusu ubabaishaji unaofanywa na TFF.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **10 MEI, 2016** | **KATIBU WA BUNGE** |